التَّمَدُّدُ الشِّيْعِيُّ

KUENEA KWA USHIA

MTUNZI
IBRAHIM AL ’AJLAANI

بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

Shukurani zote anastahiki Allah Mola wa viumbe wot, Swala na salamu zimfikie mbora wa Mitume, jamaa zake na masahaba zake wote.

Baada ya hayo:

Ndugu msomaji: Tambua kwamba kuziweka bayana njia za waovu na kufichua mipango yao ni njia inayokubalika na imetajwa katika kitabu chetu, Allah amesema:

﴿وَكَذَٰلِكَ نُفَصِّلُ ٱلۡأٓيَٰتِ وَلِتَسۡتَبِينَ سَبِيلُ ٱلۡمُجۡرِمِينَ ٥٥﴾

(Hivi ndivyo tunavyozichambua aya zetu ili ipate kubainika njia ya waovu). Al An'aam/55.

Ni jambo la manufaa sana waislamu wa kawaida kufahamu aqida za wapinzani wao, na bora zaidi waweze kuelewa mipango na njia wanazotumia mahasimu wao katika kueneza uovu wao.

Ndugu msomaji, naomba tusimame pamoja mimi na wewe tuone hatari ambayo kengele yake tayari imeshagongwa, athari zake zimeshaanza kuja juu na moto wake umeshaanza kuwaka kwa kasi kubwa. Hatari hiyo si nyengine isipokua ni hatari ya kuenea kwa Ushia katika Ulimwengu wa Kiislamu.

Ushia huu wa kiroho ni hakika sio dhana, na ni uhalisia wala sio njama. Jinamizi hili la kishia halikuacha nchi hata moja isipokua limeingia, kuanzia Japani mpaka Amerika ya Kilatini, na kutoka kaskazini mwa Ulaya hadi Afrika kwa ujumla.

Mpango huu wa Ushia umevamia Miji mbali mbali na kubomoa mambo ya kiislam, itikadi yake, historia na alama zake mbali mbali, kiasi ambacho kila mwenye uchungu ameanza kulalamikia tufani hii inayoendelea kuzidi kasi yake, katika wakati ambao mashirika na asasi za Kiislamu zimekosa uhuru na kukabiliwa na hali ngumu.

Kwa hakika jambo la kuzungumzia vita vya kiitikadi na kimawazo lina umuhimu mkubwa sawa na uvamizi wa kijeshi, hasa hasa pale tunapoona matokeo ya vita hivi na uvamizi huu ambao umepelekea uhamasishaji usioonyesha mustakbali mwema kwa umma wa kiislam.

Lakini kwanini tunatoa tahadhari ya kuenea kwa Ushia?:

Hii ni kwa sababu misingi yetu na wao inatofautiana na iko mbali kabisa mashariki na magharibi.

Ndugu msomaji, vipi tukaribiane na watu ambao wanadai kua Maimamu wa Ahlul Bait wamekingwa na makosa (Maasuumiin) na kwamba wanajua ghaibu. **Angalia: Usuulul Kaafy (J:1, Uk:165) cha Al kulayni.**

Na wamesema kuwa Qur'an imeharibiwa, na kwamba hii tuliyonayo sio Qur'an ambayo ameteremshiwa Mtume ﷺ, bali hii imebadilishwa kwa kuongezwa na kupunguzwa.**Angalia: Usuulul Kaafy: (J:1, Uk:285) cha Al Kulayni.**

Vipi tutakaribiana na watu ambao wameziachia ndimi zao kali dhidi ya Maswahaba wa Mtume ﷺ na kuwaita ni mafaasiki, kuwalaani na kuwakufurisha. **Angalia yale yaliyotajwa na Al Majlisy katika kitabu chake cha Bihaarul An-waar: (J:69, Uk:137-138).**

Kila anaekataa Uimamu wa mmoja katika Maimamu wao kumi na mbili basi Mashia wa Imaamia wanamfanya mtu huyo ni kafiri, mpotofu anastahiki kukaa milele motoni. **Angalia Haqul Yaqiin: (Uk: 189) cha Abdullah Shubbar.**

Mbali na kwamba kundi hili lina historia mbaya na mbovu dhidi ya Umma wa kiislam, Lakini pia uadui wao kwetu ni mkubwa sana, na wana chuki za ndani dhidi yetu, haupiti muda mrefu utawaona wanafanya mashambulizi na kuvunja makubaliano, mapigano na khiyana mbali mbali hufanyika.

Huu ndio uhakika na histori ya kundi hili la Imani potofu ya Kishia.

Someni historia mpate mazingatio
Wako waliopotea bila ya kujitambua

Suala la kueka wazi mwenendo wa watu hawa na njama zao za kujitanua halimaanishi kuwadhulumu au kutokuwafanyia uadilifu, kwani sisi ni Umma wa uadilifu na kuhurumiana na tusiochupa mipaka.

Ni kweli kwamba kuhimiza mapambano ya ki-makundi hakuna maslahi yoyote kwa Umma hasa katika wakati huu tulionao, na kwamba hii ni mbegu watayofaidika nayo zaidi Mayahudi wa Kizayuni na wafuasi wao.

Lakini pia kuunyamazia na kuuachia ueneaji huu wa wazi wa Ushia itakuwa ni kuwadhoofisha Ahlus Sunnah, kwani ulingano huu wa Kishia unalenga maeneo ya Sunni tu katika hatua ya kwanza.

Kwa hivyo maneno haya ni ujumbe kwa ajili ya kuufahamu mpango wa kishia wa kujitanua, na kuweza kujua hatari ya mpango huu, na kuhamasisha kupambana na mpango huu kwa njia za amani na sio kwa kutumia nguvu au vita vya kimadhebu.

Ndugu msomaji:

Wazo la kueneza Ushia lilianza mara tu baada ya Khomeini kuingia madarani, pale alipotangaza Kutanua Mapinduzi ya Kiislam.

Mpango huu wa kujitanua ulikwenda sambamba na Utawala mpya wa Faqiih ambao kwa Mashia unamaanisha kwamba: Ni wajibu kwa Mashia wa Imaamiyyah kumtii Faqiih ambae ndie naibu wa Imam anaesubiriwa.

Anasema Khomeini katika kitabu chake cha **Al Hukuumal-Islaamyah: (Uk:36)** huku akielezea Itikadi ya Utawala wa Faqiih: [Ni haki kwa Fuqahaau (Wanazuoni) bali ni wajibu kwao na ni jambo la lazima wajitahidi kuwa ni Makhalifa wa Imamu wa akher zamani,Imam anaesubiriwa, na wakamate Utawala wakiwa wa-namkaimu yeye na wafanye kazi kwa niaba yake; na kwa ajili hiyo kumtii huyu Faqiih inakuwa ni wajibu, si kwa sababu ni kama Imamu bali ni kama Nabii au Mtume].

Kwa kutumia mawazo haya Khomeini aliweza kuwadhibiti wafuasi wake popote walipo wapate kumfuata yeye na watii amri zake.

Na kwa lengo la kutanua Mapinduzi Serikali ya Khomeini imeingia katika vita na Iraq muda wa miaka minane, na baada ya kumaliza ikawa vimeacha mamia ya wafu na hasara kubwa za kiuchumi, (Na Fursi wanaichulia vita hiyo kuwa ni mlango wa kuigilia katika Ulimwengu wa Kiislam, mbali na faida wanazopata nchini Iraq katika mwelekeo wa kidini na madhehebu yao).

Serikali hii ya Mamula (Faqiih) hapo mwanzo ilikuwa inahimiza makundi ya wachache miongoni mwa Mashia kudai kujitenga na wajitawale wenyewe, na wakati huo vikaanzishwa vyama mbali mbali vya kisiasa vya kupingana na Serikali zao, ambavyo hivi sasa vina fujo na sauti kubwa Ulimwenguni, kwa mfano Hizbud Daawal Islaamiyya cha Iraq, Harakat Amal na Hizbullah huko Lebanon, na Jabhat Tahriiril Islaamiy huko Bahrein na baadae Wanaharakati wa Kihuthi huko Yemen.

Vyama hivi vimeundwa ili kutekeleza amri za Ma-Ayatola kutoka Qummi na baadae vikawa vinalingania Usafawy na Ufursy.

Lakini baada ya Fursy kushindwa kuyahamishia nje Mapinduzi yake kwa njia ya silaha wamefanya ujanja wa kuyahamisha kwa njia za kidiplomasia bila ya kutumia nguvu.

Na kwa kutumia siasa ya ustahamilivu, mipango makini, na kufanya kinachowezekana, utanuzi wa kishia umeanza kuzivamia nchi za kiislam bila kujali mipaka wala vizuizi.

Mpango huu unaungwa mkono na dola ya kishia ambayo inataka itawale kote, na inatumia nguvu zote ilizonazo pamoja na taasisi zake mbali mbali, na kutumia kiwango kikubwa kabisa cha mali ambapo inasemekana kwamba 1/5 (25%) ya mapato ya mafuta hutumika kwa ajili ya mpango huu.

Anasema Khomeini katika wasia wake wa kuwahimiza wafuasi wake kueneza Ushia: [Na jambo la kueneza Ushia si la wizara ya kidini peke yake bali ni jukumu la Wanachuoni, Makhatibu, Wandishi wa Vitabu na Wasanii,pia wizara ya mambo ya nje ina wajibu wa kueneza vipeperushi vinavyoelezea sura nzuri ya Uislam]. Al waswiya Ssiyaasiyya Lil Imaam Al Khomeini: (Uk:40).

Ama Rais wa sasa wa Iran Ahmad Nijaad yeye ametangaza wazi kuwa lengo la Utawala wa Iran ni kusambaza Ushia ulimwenguni, na kupeperusha bendera ya Mahdil Muntadhar na kuitangaza.

Amesema: [Jukumu la kuitangaza kazi hii ni la Serikali ya Iran]. Nukuu kutoka mtandao wa Mufakiratul Islaam].

Mwanazuoni mmoja wa kishia ameeleza katika mazungumzo yake na kituo cha televisheni cha (Al Mustaqilla) tarehe 4/1/1428H: [Uongozi wa kishia wa Qummi na Najaf unafanya jitihada za kutaka kutawala eneo lote la Hijazi, Sham,Yemen na Iraq, na lengo la Utawala wa kidini ni kukamata uongozi wa Ulimwengu wote wa Kiislam, na kwamba kueneza Ushia hakuna mipaka na wanataka kueneza katika maeneo yote.

AMA MIPANGO NA NJIA WANAZOTUMIA KATIKA KUENEZA USHIA NA JINSI WALIVYOFANIKIWA:

NJIA YA KWANZA KABISA**: Ni kutoa kauli mbiu ya kuwapenda Ahlul Bait** na kuyapa madhehebu yao jina la Madhehebu ya Ahlul Bait na kuifanya kauli mbiu yao iwe ni kuwapenda Ahlul Bait, kutaja fadhila zao na kuzitilia nguvu haki zao tu.

Kauli mbiu hii Shia wanaichukulia kama ni daraja la kuvukia kuelekea kwenye kuwatukuza na kuwaabudu, kisha kuwatukana wale wanaodaiwa na wao Mashia kwamba wamewadhulumu Ahlul Bait, na kuwapora haki yao ambao ni Maswahaba wa Mtume ﷺ, kisha hatua inayofatia ni kuwasema vibaya, kuwalaani na kuwakufurisha.

Kwa hivyo kauli mbiu hii ya kuwapenda Jamaa wa Mtume..ni mbinu tu ya kueneza madhehebu ya Ushia na kuupamba ili upate kukubalika.

Na ndio maana Jumuia za kidaawa, misada na hata za kisiasa

huwa zinapewa majina ya Ahlul Bait ili kuyatangaza madhehebu haya yapate kukubalika.

Mashia wameyafanya makaburi ya Ahlul Bait kuwa ni maeneo ya ziara, wameyajengea Maquba na kufanya ibada mbali mbali hapo za kibidaa na ukafiri. Pia hujengwa katika maeneo hayo Majamati (Husayniyya) na hununuwa ardhi zilizo karibu na eneo hilo ili eneo lote hilo liwe ni la kishia.

❑ NA MIONGONI MWA NJIA ZAO KATIKA KUENEZA MADHEHEBU YAO NI: **Wito wa usuluhishi wa Kimadhehebu baina ya Masunni na Mashia.**

Wito huu undani wake ni kukubaliana na Ushia na kuuona kuwa ni Madhehebu sahihi, na kurahisisha njia ya kukubalika na kufaa kufuatwa.

Mbinu hii kwa bahati mbaya imewawezesha Mashia kuingia kaatika nchi za Masunni wanavyotaka, na imewapa uwezo pia wa kufungua Maraakiz na mashirika ya usambazaji na kueneza Madhehebu yao.

Na kupinga itikadi zao hizi potofu na mafundisho yao yaliyosheheni ukafiri hili kwao huonekana kuwa ni Mpasuko unaotishia kuvunjika kwa umoja wa kiislamu.

Lakini Masunni wana haki ya kujiuliza: Je Mamula wa Iran wataruhusu kulingania Usunni katika maeneo ya Kishia? Na je wafursi watanyamaza kimya wakiiona Iran inaingia katika Usunni? Je watakubaliana na harakati kama hizi?

Laa wallah hapana, Utawala unazuwia kabisa kufundisha itikadi ya Kisunni hata kwenye Mashule ya dini.

Utawala wa Iran ambao unadai kuhimiza umoja na mshikamano (Utawala huo) ndio unaowauwa Maulamaa wa kisunni, na ndio unaowaangamiza waarabu wa Ahwaaz, kuvunja miskiti, kufunga Mashule na kuwasaka Masheikh wa Kisunni.

Bila shaka sisi Ahlus Sunna haiwezekani kuwa karibu na watu ambao wanazipinga nguzo za kiislamu, wanaabudia makaburi na kufanya juhudi ya kuenaza bidaa.

❑ NA MIONGONI MWA NJIA ZAO KATIKA KUENEZA MADHEHEBU YAO NI:

Kutoa ufadhili wa masomo kwa wingi, na kuchukua mamia kwa maelfu ya wanafunzi kutoka maeneo mbali mbali na kuwapokea katika vyuo ya kielimu huko Tehran, Qummi, Mas'hhad na Tibriizy.

Na serikali ya Mamula ndio inayodhamini gharama zote za masomo yao na mpaka kuwaozesha wake.

Na lengo kuu la Scholarship hizi ni kuwaingiza katika Ushia kisha waeneze katika maeneo yao watakaporudi kwao.

Na hapo usiulize kuhusu uzalendo wao, kwani wao tayari wameshapikwa miaka na miaka na kuambiwa kwamba serikali zote ni za dhulma na si za halali kwa sababu hazifuati muongozo wa Faqiih au kama wanavyodai hazifuati muongozo wa dini asilia ya Muhammad.

Na katika mbinu zao pia: Ni kupeleka Maduati na walimu sehemu mbali mbali kwa lengo la kueneza Ushia hasa hasa katika maeneo ya mbali na maeneo ambayo kuna waislamu wachache.

Baadhi ya magazeti ya kigeni yameeleza kuwa: Serikali ya Iran baada ya kusambaratika kwa Muungano wa Kisovieti ilipeleka mamia ya walimu katika Jamhuri zilizojitenga.

Gazeti likaongeza kuwa jambo hili limeigharimu Iran mabilioni ya Dola.

❑ NA MIONGONI MWA NJIA ZAO KATIKA KUENEZA MADHEHEBU YAO:

Kunufaika na Ubalozi wa Iran katika kila nchi,mpaka kwenye kitengo cha Utamaduni imewekwa wizara ndogo kwa ajili ya kulingania kwenye Ushia,kwa kupitia wakazi wa ki-shia,kwa kufuatilia kesi zao, kukutea haki zao, na kuwapatia habari za dini na siasa ya ki-shia; kwa hiyo katika Ubalozi wowote wa Iran kuna masheikh wenye vilemba ambao ni walinganizi wa Ushia.

❑ NA MIONGONI MWA NJIA ZAO KATIKA KUENEZA MADHEHEBU YAO:

Kutumia silaha ya Mali, kuwadanganya watu na starehe za ki-dunia,na kuwanunua watu mashuhuri na wazee wa Makabila kwa kuwapatia Mali nyingi na mgao maalumu (donge nono) ili kuwaingiza katika madhehebu ya Ushia, na kuwa taswira ya kwamba hakuna tafauti katika Uislamu baina ya Shia na Sunni.

Na sio siri (ewe ndugu msomaji) ya kwamba Ushia umeenea katika nchi ya Iraq na Sirya kupitia mlango wa watu mashuhuri, na wazee wa Makabila.**Angalia kitabu: [Tahdhiirul bariyyah min nashaatwi Sshia fii Suuriyyah].**

❑ NA MIONGONI MWA NJIA ZAO KATIKA KUENEZA MADHEHEBU YAO:

Kufuatilia maeneo yenye ujinga mwingi (yasiyo na elimu), na

sehemu zenye umasikini, na kuwekeza katika maeneo hayo kwa kujenga Hospitali,kusaidia masikini,kuboresha maisha na kutoa misada mbalimbali,lakini ni pamoja na kuhubiri madhehebu ya Ushia.

Watu wengi walio masikini na wanyonge wameingia katika dini ya Ushia kupitia chini ya kivuli cha upendo wa Kiislamu, na kuwapenda Ahlul Bayt (jamaa wa Mtume ﷺ).

- NA MIONGONI MWA NJIA ZAO KATIKA KUENEZA MADHEHEBU YAO:

Madai ya kufuatilia kadhia za waislamu, na kuwa na mtazamo hasi (uadui) kwa Mayahudi na Wazayuni (Zionism),na siasa za Magharibi,jambo ambalo limeleta athari kubwa kuwatakasa Mashia katika Ulimwengu wa Kiislamu, na kuungwa mkono na watu wenye kudhulumiwa.

Ama mbinu anazofanya kiongozi wa Iran (Ali Khamenei) kuhusu kadhia ya Palestina ni kufurahisha hisia za watu tu, kupata maslahi kwa Madhehebu (ya kishia) na kuendesha maisha ya Ki-siasa.

Amesema Spika wa Bunge la Iran: [Nguvu ya ki-Mali inayotoa Nchi ya Iran kusaidia Nchi za Kiislamu ni kwa ajili ya maslahi ya Taifa la Iran]. **Rejea: (Mauqi' swahiifatil Akhbaaril ikturuuny) gazeti la siku ya ijumaa June 2008**[m].

Huku ni kukiri kwa mmoja wa Wanasiasa wa Iran kwamba juhudi zinazofanywa na Iran ni kwa ajili ya maslahi yake tu, wala si kwa maslahi ya Umma wa Kiislamu.

- AMA NAFASI YA KISIASA (INAVYOTUMIKA) KATI-KA KUENEZA USHIA NI:

Kutoa ushirikiano kwa mataifa ya kigeni katika kupiga (na kuziangusha) Dola za Ki-sunni zinazopambana na Ushia; kwa hiyo ilisimama Serikali ya Iran (ambayo kwa miaka mingi wanapiga kelele masheikh wao wenye vilemba kwa kumlani shetani mkubwa Amerika) kusaidiana na Serikali ya kigeni (Jeshi la Marekani) kwa ajili ya kuingusha Dola ya Iraq, na kabla ya hapo (pia alifanya hivyo) kwa Dola ya Afghanistan, amelibainisha hilo waziwazi Naibu msatahafu wa Rais wa Iran Muhammad Abtwahiy: [Bila Iran basi Amerika isingeweza kuitawala kwa nguvu Nchi ya Iraq, na lau si Iran Amerika isingetawala ki-mabavu Nchini Afghanistan].**Rejea kitabu: (Maadha ta'rifu an Hizbullah: uk: 208).**